



Kuleta pamoja mashirika yanayojihusisha na elimu.

Wewe ni mtaalamu/mbobezi katika jamii yako. TeachUNITED ni mtaalamu/mbobezi katika ufundishaji wa wakufunzi. Kwa kushirikiana pamoja, tunakuandaa wewe kufundisha wakufunzi katika mtandao wako wa shule kwenye mbinu za ufundishaji zenye matokeo ili kuhakikisha kila mtoto anapata elimu yenye ubora wa juu.



MPANGILIO WA UTEKELEZAJI

AWAMU YA KWANZA

Wafanyakazi wa taasisi wanatengeneza kikundi na kupokea yafuatayo;

- Fursa ya kuingia kwenye kozi ya mtandaoni inayotolewa na TeachUNITED
- Mafunzo ya mmoja-mmoja kutoka kwa Mkufunzi wa TeachUNITED
- Warsha na Semina za mtandaoni zinazojenga jumuiya

Kikundi kitapata ujuzi mbalimbali na kujiamini kunakohitajika kufundisha wafundishaji wengine kwenye shule mnazofanya nazo kazi kuhusiana na jinsi ya kutekeleza mikakati ikiwemo Mtazamo Chanya/wa Ukuaji, Ujifunzaji wa Kipekee, Ushirikishaji wa Mwanafunzi, na Mtaumizi sahihi ya Data za Mwanafunzi.

AWAMU YA PILI

Kikundi kinafundisha programu shuleni.

Watapokea kila kinachohitajika kusaidia mafunzo ya kitaaluma kwa shule nzima ikiwemo;


1. Mfumo wa kubuni mikutano ya mtandaoni
2. "Notes"
3. Ratiba
4. Machapisho
5. Mazoezi ya Kusaidia Tathmini

Wakufunzi wa TeachUNITED wataendelea kutoa msaada na mafunzo na ushauri.

TeachUNITED ni taasisi ya kimataifa isiyo ya kiserikali ambayo imejikita katika kuwainua walimu kupitia ukufunzi mahiri, mikakati iliyohakikiwa, na ujifunzaji wa kipekee. Walimu wanapata mapinduzi kwenye ufundishaji na ujifunzaji, na matokeo bora ya mwanafunzi.



Wasiliana nasi kupitia: partnerships@teachunited.org



MAELEZO YA PROGRAMU

Washiriki	Wafanyakazi wa taasisi husika, Walimu na/au Wakufunzi
Muda wa Mafunzo	Inategemea na mahitaji ya taasisi yako, lakini kikawaida inahitaji kati ya miezi 6-12 kwa mafunzo ya awali.
Ratiba	Wafanyakazi wahusika pamoja na walimu watatumia saa 10-12 kwa kila kipengele katika SAP (School Accelerator Program) ambayo inajumuisha masomo mtandaoni, mafunzo ya vitendo, kufundisha na mikutano ya mtandaoni.

MUUNDO WA MAFUNZO

- Fursa ya kuingia kwenye kozi ya mafunzo mtandaoni
- Mikutano miwili kwa kila kipengele, jumla mikutano minane kwa Programu
- Msaada kwa Jumuiya ya Ujifunzaji wa Kitaaluma (PLCs) shuleni katika kipindi cha mara mbili kwa wiki, au kila baada ya wiki mbili.
- Mafunzo ya mmoja-mmoja, mara moja au mara mbili kwa kila kipengele, jumla mafunzo 6-8 kwa program
- Fursa ya tathmini ya Kipekee na Mrejesho katika kipindi chote cha Mafunzo ya Mtandaoni

MFANO WA MATOKEO YA MAFUNZO



- Kupata uzoefu katika Kupima Matokeo na Kufanya Tathmini; Kuelewa jinsi ambavyo data huelezea ufundishaji na kujifunza; Jifunze jinsi ya kupima matokeo ya ufundishaji/ukufunzi.
- Kusaidia wakufunzi kubuni, kuunda na kutathmini masomo kwa ajili ya ushirikishaji wa mwanafunzi na matokeo.
- Tambua/Elewa changamoto za mara kwa mara katika ujifunzaji wa kipekee na jinsi ya kujenga uwezo katika kuzikabili katika ngazi ya ujenjaji.



Wasiliana nasi kupitia: partnerships@teachunited.org